


Wajibika na Zuia Majanga Yasababishwayo na Uendeshaji Mbaya



Zima vifaa vyote vya umeme na viweke mbali kabla ya kuanza kuendesha.

Ni marufuku kuweka simu yako katika kofia au kitambaa cha kichwani ili kuongea wakati unaendesha.

Kuwa dereva mzuri wa kuigwa kwa madereva wengine. Ukiwa abiria msaidie dereva kupiga simu au kuandika ujumbe mfupi kwa niaba yake, ili umakini wake ubakie kwenye kuendesha kwa usalama. Ongea na watoto kuhusu kuendesha gari kwa kuwajibika.

Funga mkanda wakati wote na kuwaweka watoto kwenye viti vyao salama ili uwe salama kutokana na madereva wasio salama.

Watembea kwa miguu na waendesha baisikeli wote wanatakiwa kuangalia mazingira yanayowazunguka bila kutumia vifaa vya umeme. Chanzo: Imerekebishwa 9/6/18 <https://www.nhtsa.gov/press-releases/us-dot-and-nhtsa-kick-5th-annual-u-drive-u-text-u-pay-campaign>

Ukiandika ujumbe mfupi wakati unaendesha, kuna uwezekano wa mara 20 kupata ajali kuliko anayeendesha gari vizuri.

- Watu 3450 walikufa kwenye ajali iliyohusisha madereva waliopotoshwa 2016.
- Waenda kwa miguu, waendesha baisikeli na wengine 562 walikufa kwa ajali zilizosababishwa na madereva waliopotoshwa 2016.
- Asilimia 70 ya madereva waliopotoshwa waliohusika katika ajali mbaya walikuwa wanaume, kulinganisha na asilimia 74 ya ajali zote mbaya.
- Matumizi ya simu za mkononi wakati wa kuendesha ni kubwa kati ya madereva wa miaka 15-29.
- Madereva wanawake wenye simu wamekuwa na uwezekano mkubwa wa kuhusika na ajali mbaya za uendeshaji uliopotoshwa kulinganisha na wanaume kila mwaka toka 2012.
- Asilimia 9 ya madereva wote wa miaka 15-19 waliohusika kwenye ajali mbaya waliripotiwa kuwa madereva waliopotoshwa. (Chanzo: Imerekebishwa 9/6/18 <https://www.nhtsa.gov/press-releases/us-dot-and-nhtsa-kick-5th-annual-u-drive-u-text-u-pay-campaign>)

Vikwazo vya Kisheria Vinaweza Kuanzia Kulipa Fidia Na Malipo kwa Madhara Makubwa ya Uhamiaji.

Ni kinyume cha sheria kutumia simu za mkononi au kifaa kidogo cha umeme wakati unaendesha. Shughuli haramu zinajumuisha kubeba kifaa kidogo cha umeme na kuongea kwenye simu ya mkononi inayojumuisha, kutuma, kusoma, kufikia, kutumia mtandao, kuhamisha, kuhifadhi, au kutafuta data za umeme kama vile barua pepe, au ujumbe mfupi, au kuchukua kurasa za mtandao, au kutumia mtandao kutuma picha au kucheza michezo.

Maondoleo kwa sheria, inamaanisha, imeruhusiwa kisheria ku: Piga 911 au wasiliana na wanaotoa matiba, wazima moto au polisi kuhusu dharura. Kwa dereva kutumia simu ya mkononi, ambayo inamruhusu mtumiaji kuwasiliana bila ya kutumia mkono wowote. Kutumia kifaa cha umeme cha mkononi ambacho kimewekwa kwenye uso wa gari. Kutumia kifaa cha GPS ambacho kimeunganishwa kwenye gari.

Unaweza kupata tiketi ya trafiki na kutozwa fidia na malipo kwa kutumia kifaa kidogo cha umeme wakati unaendesha. Hukumu ya matumizi ya simu ya mkononi, kutumia kifaa kidogo cha umeme au kuandika ukiukwaji pia utaleta matokeo ya kuongezewa rekodi ya pointi kwenye leseni yako ya DMV. Kama utapokea pointi 11 ndani ya kipindi cha miezi 18, leseni yako ya udereva inaweza kusimamishwa. Kujifunza zaidi, tazama [About the NYS Driver Point System](http://dmv.ny.gov/tickets/about-nys-driver-point-system), <http://dmv.ny.gov/tickets/about-nys-driver-point-system>.

TS.DD. Swahili. Distracted Driving (Rev. 2019)